

2. UFAHAMU

Soma taarifa ifuatayo halafu ujiu maswali

UMOJA NA UTANGAMANO WA KITAIFA

Taifa ni jamii ya watu wanaoishi pamoja na kuunganika kihistoria na kitamaduni chini ya serikali moja. Muunganiko huu hutokea kinasibu na watu kujikuta chini ya himaya moja. Umoja na utangamano katika taifa hutokana na mambo kadha wa kadha.

Kwanza kabisa ni ushirikiano baina ya wanajamii wenyewe. Umoja wao huletwa na lugha wanayotumia. Hapa nchini Kenya Kiswahili kimechangia pakubwa katika kuleta utangamano. Luhga ya Kiswahili inazungumzwa kote nchini. Wananchi kutoka sehemu tofauti za nchi wanaweza kuwasiliana bila shida yoyote.

Pili, utawala wa serikali ya kitaifa huleta utangamano wa jamii katika nchi. Huduma za serikali hutolewa kwa wote bila ya ubaguzi. Nchi inapokuwa chini ya kiongozi aliyechaguliwa na wananchi hufanikisha umoja.

Jambo lingine ambalo huleta utangamano wa kitaifa, ni kuweko kwa sera inayoongoza maazimio na malengo ya taifa. Viongozi na wananchi wote hujitahidi kuchangia katika kuyafikia maazimio na malengo ya taifa lao.

Utamaduni wa nchi nao ni muhimu katika kuleta umoja wa kitaifa. Mila, itikadi na kaida zenye manufaa na zinazokubalika na jamii hufanikisha kutambulisha taifa. Hivyo wananchi kupigania kwa jino na ukucha kuhifadhi utamaduni wao. Kwa mfano: sanaa za uigizaji na uimbaji nchini Kenya husaidia kutomelea umoja huu. Tamasha hizi ni chombo muhimu cha utangamano. Mfumo sawa wa elimu nchini ni njia nyingine ya kuimarisha umoja wa kitaifa.

Wafanyibiashara wanaposafiri kutoka sehemu moja ya nchi hadi nyingine hutangamana na wananchi wenzao wanapouza au kununua bidhaa na huduma. Utangamano huo hukuza umoja wao.

Maswali

a) Eleza maana ya taifa. (al 2)

.....
.....

b) Eleza umuhimu wa Kiswahili nchini Kenya. (al2)

.....
.....

c) Taja mambo manne ambayo huleta umoja wa kitaifa. (al4)

.....
.....
.....
.....

d) Eleza maana ya maneno yafuatayo kwa mujibu wa kifungu hiki. (al 2)

i) Utangamano.....

ii) Utamaduni

3. Matumizi ya lugha (al. 30)

a) Taja sifa mbili mbili za sauti zifuatazo. (al. 4)

i) /u/.....

ii) /e/.....

b) Yaja sauti mbili mbili ambazo ni, (al. 6)

i) Vipasuo.....

ii) Nazali.....

iii) Vikwamizo.....

c) Pambanua aina za maneno katika sentensi ifuatayo. (al. 2^{1/2})

Maharagwe yalivunwa na kutiwa ghalani.

.....
.....

d) Panga maneno haya vizuri ili yaunde sentensi sahihi. (al. 2)

Hodari Yule mwanamuziki nchi amezuru nyingi Afrika za.

.....
.....

e) Tunga sentensi moja moja kubainisha maana ya maneno yafuatayo; (al.2)

i) Paa

.....
.....

ii) Shuka

.....
.....

f) Kanusha sentensi ifuatayo; (al. 2)

Mwalimu anasahihisha kitabu cha mwanafunzi.

g) Andika sentensi ifuatayo upya ukizigatia maagizo kwenye mambano. (al. 2)
Mazingira yamehifadhiwa. (hali ya mazoea)

h) Maneno yafuatayo hupatikana katika ngeli zipi? (al. 2)

1. Manukato.....

2. Sukari.....

i) Tofautisha sentensi hizi. (al. 4)

1. Gari liliibwa

2. Gari liliibiwa

j) Kamilisha sentensi zifuatazo kwa kutumia vitenzi vilivyo katakia mambano.(al. 2)

i) Sauti hii ilina fuudi wa kihindi. (shone)

ii) Yuko wapi Yule mgonjwa aliye..... hapa? (leta)

k) Eleza maana ya msamiati ufuatao wa ushairi. (al. 2^{1/2})

i) Ubeti

ii) Mizani

iii) Mshororo

iv) Ukwapi

.....
.....
v) Dhamira
.....
.....

4.ISIMUJAMII (al 10)

a) Eleza maana ya;
i) Isimu
.....
.....

iii) Jamii
.....
.....

iv) Isimujamii
.....
.....

v) Sajili
.....
.....

vi) Lafudhi
.....
.....

5.FASIHI SIMULIZI. (al 10)

a) Eleza maana ya fasihi. (al. 2)
.....
.....

b) Toa sifa nne ili kutofautisha fasihi andishi na fasihi simulizi. (al. 8)

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....